

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**



**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**FUNGU 80**

**MKOA WA Mtwara**

**MAELEZO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2015/16,  
NUSU MWAKA 2016/17 NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI  
YA MWAKA 2017/2018 KWA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA  
UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA**

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,  
S.L.P 544,  
**MTWARA**  
Simu/Nukushi: 023 – 2333194  
Barua pepe: [rc@mtwara.go.tz](mailto:rc@mtwara.go.tz)/[ras@mtwara.go.tz](mailto:ras@mtwara.go.tz)  
Tovuti: [www.mtwara.go.tz](http://www.mtwara.go.tz)

**Machi, 2017**

## **1.0 UTANGULIZI**

Taarifa hii inaelezea kwa muhtasari utekelezaji wa bajeti ya Sekretarieti ya Mkoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka 2015/2016, nusu mwaka 2016/2017 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2017/2018. Aidha, utekelezaji wa bajeti ya Sekretarieti ya Mkoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa unaongozwa na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Malengo ya Maendeleo Endelevu, Ilani ya Uchaguzi ya chama tawala (CCM) 2015, Mipango mikakati ya Sekretarieti ya Mkoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mpango wa Matokeo Makubwa sasa (BRN), hotuba ya Mhe.Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wa kuzindua Bunge la 11 na mipango mbalimbali ya kitaifa.

## **2.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA 2015/2016**

### **2.1 MADUHULI YA MKOA NA MAKUSANYO YA HALMASHAURI**

#### **2.1.1 Makadirio na Makusanyo ya Sekretarieti ya Mkoa kwa mwaka 2015/16**

Katika kipindi cha mwaka 2015/16 Sekretarieti ya Mkoa ilitarajia kukusanya jumla ya shilingi **541,000.00** kutoka chanzo cha kodi ya pango katika nyumba tano za Serikali kama mapato ya Serikali yanayokwenda moja kwa moja Hazina. Hadi Juni, 2016 jumla ya shilingi **541,000.00** zilikusanywa sawa na asilimia **100.00** ya makadirio.

#### **2.1.2 Makadirio na Makusanyo ya Halmashauri kwa mwaka 2015/16**

Katika kipindi cha mwaka 2015/16 Halmashauri zilikadiria kukusanya mapato ya ndani yenye jumla ya shilingi **21,099,534,000.00** kutoka vyanzo mbalimbali vya ndani. Hadi Juni, 2016 jumla ya shilingi **16,896,322,000.00** zilikusanywa sawa na **80.08%** ya makadirio. Jedwali Na.1 linaonesha mchanganuo wake.

**Jedwali Na.1: Makadirio na Makusanyo ya Halmashauri hadi Juni, 2016**

HALMASHAURI	MAKADIRIO	MAKUSANYO HADI JUNI, 2016			
		MAKUSANYO YASIYOLINDWA	MAKUSANYO LINDWA	JUMLA	%
Mtwara Mikindani	3,205,204,000	2,592,380,000	143,146,000	2,735,526,000	85.35
Mtwara	1,631,242,000	1,283,855,000	42,789,000	1,326,644,000	81.33
Newala	2,996,000,000	1,731,777,000	849,717,000	2,581,494,000	86.16
Nanyumbu	1,800,372,000	1,258,864,000	309,419,000	1,568,283,000	87.11
Masasi	3,778,152,000	1,607,700,000	1,583,752,000	3,191,452,000	84.47
Masasi Mji	1,872,229,000	885,326,000	520,470,000	1,405,796,000	75.09
Tandahimba	4,773,334,000	2,222,403,000	1,219,992,000	3,442,395,000	72.12
Nanyamba Mji	1,043,001,000	630,847,000	13,885,000	644,732,000	61.82
<b>JUMLA</b>	<b>21,099,534,000</b>	<b>12,213,152,000</b>	<b>4,683,170,000</b>	<b>16,896,322,000</b>	<b>80.08</b>

**Nyongeza:** Makusanyo lindwa ni mapato yanayojumuisha vyanzo vya ada ya huduma (user fee), mfuko wa afya ya jamii (CHF), mfuko wa elimu na export levy. Matumizi ya fedha hizi huzingatia sheria ya CHF, Mfuko wa elimu na miongozo ya cost sharing na export levy.

Halmashauri hazikuweza kufikia malengo ya makusanyo kutokana na;

- Kushuka kwa bei za mazao.
- Kuchelewa kuidhinishwa kwa sheria ndogo.
- Kuondolewa kwa ada mashuleni.
- Mabadiliko ya hali ya hewa iliyoathiri uzalishaji wa mazao.
- Vyama vya msingi kutolipa ushuru kwa wakati.
- Kufungwa kwa baadhi ya makampuniya yanayoshughulika na utafutaji wa gesi.

Matumizi mapato ya ndani katika miradi ya maendeleo kwa makusanyo yasiyolindwa ni kama inavyooneshwa katika jedwali namba 2.

**Jedwali Na.2: Matumizi ya makusanyo yasiyolindwa kwa mwaka 2015/2016**

HALMASHAURI	MAKUSANYO YASIYOLINDWA	Wanawake na Vijana (10%)				Miradi ya Maendeleo (50%)			
		Takiwa	%	Tolewa	%	Takiwa	%	Tolewa	%
Mtwara MC	2,592,380,000	259,238,000	10	140,000,000	54.00	1,296,190,000	50	1,111,000,000	85.71
Mtwara	1,283,855,000	128,385,500	10	39,912,000	31.09	641,927,500	50	364,412,000	56.77
Newala	1,731,777,000	173,177,700	10	99,000,000	57.17	865,888,500	50	743,392,000	85.85
Nanyumbu	1,258,864,000	125,886,400	10	125,886,000	100.00	629,432,000	50	629,432,000	100.00
Masasi	1,607,700,000	160,770,000	10	160,770,000	100.00	803,850,000	50	803,850,000	100.00
Masasi TC	885,326,000	88,532,600	10	7,389,000	8.35	442,663,000	50	196,442,000	44.38
Tandahimba	2,222,403,000	222,240,300	10	222,240,000	100.00	1,111,201,500	50	1,078,328,000	97.04
Nanyamba TC	630,847,000	63,084,700	10	47,000,000	74.50	315,423,500	50	212,825,000	67.47
<b>JUMLA</b>	<b>12,213,152,000</b>	<b>1,221,315,200</b>	<b>10</b>	<b>851,957,000</b>	<b>69.75</b>	<b>6,106,576,000</b>	<b>50</b>	<b>5,139,681,000</b>	<b>84.16</b>

**2.2 FEDHA ZA RUZUKU KWA MATUMIZI YA KAWAIDA MWAKA 2015/2016**

**2.2.1 Fedha zilizoidhinishwa na kutolewa kwa Sekretarieti ya Mkoa mwaka 2015/16**

Katika mwaka 2015/16 Sekretarieti ya Mkoa iliidhinishwa jumla ya shilingi **7,939,998,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida ili kugharamia maeneo ya mishahara na matumizi mengineyo. Fedha zilizotolewa hadi Juni, 2016 ni jumla ya shilingi **6,245,155,000.00** sawa na **78.65%** ya bajeti iliyoidhinishwa. Aidha, kiasi kilichotumika ni shilingi **6,245,155,000.00** sawa na **100.00%** ya fedha zilizotolewa. Jedwali na.3 linaonesha mchanganuo wake.

**Jedwali Na.3: Bajeti, Fedha zilizotolewa na kutumika hadi Juni, 2016**

KASMA	BAJETI	FEDHA TOLEWA		FEDHA TUMIKA	
		KIASI	%	KIASI	%
Mishahara	6,360,640,000	5,186,641,000	81.54	5,186,641,000	<b>100.00</b>
Matumizi Mengineyo	1,579,358,000	1,058,514,000	67.02	1,058,514,000	<b>100.00</b>
<b>JUMLA</b>	<b>7,939,998,000</b>	<b>6,245,155,000</b>	<b>78.65</b>	<b>6,245,155,000</b>	<b>100.00</b>

## 2.2.2 Fedha zilizoidhinishwa na kutolewa kwa Halmashauri mwaka 2015/16

Katika mwaka 2015/16 Halmashauri ziliidhinishwa fedha za ruzuku jumla ya shilingi **122,468,548,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida ili kugharamia maeneo ya mishahara na matumizi mengineyo. Fedha zilizotolewa hadi Juni, 2016 ni jumla ya shilingi **115,195,597,000.00** sawa na asilimia **94.06**. Aidha, kiasi kilichotumika ni shilingi **115,195,597,000.00** sawa na **100.00%** ya fedha zilizopokelewa. Jedwali Na.4 na 5 yanaonesha michanganuo yake.

**Jedwali Na.4: Bajeti na Mapokezi ya fedha za Matumizi ya Kawaida hadi Juni, 2016**

HALMASHAURI	BAJETI		FEDHA TOLEWA			
	MISHAHARA	MATUMIZI MENGINEYO	MISHAHARA	%	MATUMIZI MENGINEYO	%
Mtwara Mikindani	13,718,979,000	1,475,351,000	12,822,247,000	93.40	721,806,000	48.92
Masasi Mji	11,022,410,000	1,112,452,000	11,256,168,000	102.12	514,972,000	49.26
Mtwara	18,504,714,000	1,875,922,000	17,580,118,000	95.00	799,281,000	42.61
Masasi	20,133,814,000	2,436,761,000	18,044,491,000	89.62	1,190,069,000	48.84
Nanyumbu	11,275,735,000	1,170,557,000	12,546,496,000	111.27	492,793,000	42.10
Newala	17,072,549,000	1,610,226,000	18,079,728,000	105.90	714,270,000	44.36
Tandahimba	19,417,929,000	1,641,149,000	19,592,481,000	100.90	840,677,000	51.22
<b>JUMLA</b>	<b>111,146,130,000</b>	<b>11,322,418,000</b>	<b>109,921,729,000</b>	<b>98.90</b>	<b>5,273,868,000</b>	<b>46.58</b>
<b>JUMLA KUU</b>	<b>122,468,548,000</b>		<b>115,195,597,000</b>			<b>94.06</b>

**Jedwali Na.5: Fedha zilizotolewa na kutumika kwa Matumizi ya kawaida hadi Juni, 2016**

HALMASHAURI	FEDHA ZILIZOTOLEWA		FEDHA ZILIZOTUMIKA			
	MISHAHARA	MATUMIZI MENGINEYO	MISHAHARA	%	MATUMIZI MENGINEYO	%
Mtwara Mikindani	12,822,247,000	721,806,000	12,822,247,000	100.00	721,806,000	100.00
Masasi Mji	11,256,168,000	514,972,000	11,256,168,000	100.00	514,972,000	100.00
Mtwara	17,580,118,000	799,281,000	17,580,118,000	100.00	799,281,000	100.00
Masasi	18,044,491,000	1,190,069,000	18,044,491,000	100.00	1,190,069,000	100.00
Nanyumbu	12,546,496,000	492,793,000	12,546,496,000	100.00	492,793,000	100.00
Newala	18,079,728,000	714,270,000	18,079,728,000	100.00	714,270,000	100.00
Tandahimba	19,592,481,000	840,677,000	19,592,481,000	100.00	840,677,000	100.00
<b>JUMLA</b>	<b>109,921,729,000</b>	<b>5,273,868,000</b>	<b>109,921,729,000</b>	<b>100.00</b>	<b>5,273,868,000</b>	<b>100.00</b>
<b>JUMLA KUU</b>	<b>115,195,597,000</b>		<b>115,195,597,000</b>			<b>100.00</b>

### **2.2.3 Shughuli zilizotekelezwa hadi Juni, 2016**

Orodha ya baadhi ya shughuli zilizotekelezwa na Sekretarieti ya Mkoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa hadi Juni, 2016 ni pamoja na;

#### **a) Sekretarieti ya Mkoa**

- Kusimamia masuala ya ulinzi na usalama ndani ya Mkoa.
- Kuendesha vikao vya mbalimbali vya kisheria.
- Kutoa ushauri wa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa.
- Kuratibu shughuli mbalimbali za Serikali za kila siku za kutoa huduma kwa wananchi.
- Kulipa mishahara kwa watumishi.
- Kuratibu uendeshaji wa mitihani ya elimu msingi na sekondari.
- Kuratibu ziara za viongozi mbalimbali wa Mkoa na kitaifa.
- Kufanya ufuatiliaji wa shughuli zilizotekelezwa na Halmashauri.
- Kutoa huduma za tiba na kinga katika hospitali ya Mkoa.
- Ufuatiliaji wa uandikishaji wa wanafunzi kwa shule za msingi na sekondari.

#### **b) Mamlaka za Serikali za Mitaa**

- Kulipa mishahara kwa watumishi wote.
- Kufanya ufuatiliaji na usimamizi wa shughuli zilizotekelezwa katika Kata, Vijiji/Mitaa na Vitongoji.
- Kutoa huduma mbalimbali za kila siku kwa wananchi.
- Kuendesha vikao vya mbalimbali vya kisheria.
- Uendeshaji wa mitihani ya elimu msingi na sekondari.

## 2.3 FEDHA ZA RUZUKU KWA MIRADI YA MAENDELEO MWAKA 2015/2016

### 2.3.1 Fedha zilizoidhinishwa na kutolewa kwa Sekretarieti ya Mkoa mwaka 2015/16

Katika mwaka wa fedha 2015/16 Sekretarieti ya Mkoa iliidhinishwa jumla ya shilingi **972,188,000.00** ili kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi **798,377,000.00 (82.12%)** ni fedha za ndani na shilingi **173,811,000.00 (17.88%)** ni fedha za nje. Hadi kufikia Juni, 2016 jumla ya shilingi **465,793,000.00** zilitolewa sawa na asilimia **47.91**. Aidha, kiasi kilichotumika ni shilingi **465,793,000.00** sawa na **100.00%** ya fedha zilizopokelewa. Jedwali Na.6 linaonesha mchanganuo wake.

**Jedwali Na.6. Bajeti, Fedha zilizotolewa na kutumika hadi Juni, 2016**

KASMA	BAJETI	FEDHA TOLEWA		FEDHA TUMIKA	
		KIASI	%	KIASI	%
Fedha za Ndani	798,377,000	0	0.00	0	0.00
Fedha za Nje	173,811,000	465,793,000	267.98	465,793,000	100.00
<b>JUMLA</b>	<b>972,188,000</b>	<b>465,793,000</b>	<b>47.91</b>	<b>465,793,000</b>	<b>100.00</b>

### 2.3.2 Fedha zilizoidhinishwa na kutolewa kwa Halmashauri mwaka 2015/16

Katika mwaka wa fedha 2015/16 Halmashauri ziliidhinishwa jumla ya shilingi **12,626,184,000.00** ili kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi **8,290,351,000.00 (65.66%)** ni fedha za ndani na shilingi **4,335,833,000.00 (34.34%)** ni fedha za nje. Hadi kufikia Juni, 2016 jumla ya shilingi **5,159,436,000.00** zilitolewa sawa na **40.86%**. Aidha, kiasi kilichotumika ni shilingi **3,469,425,000.00** sawa na **67.24%** ya fedha zilizopokelewa. Jedwali Na.7 na 8 yanaonesha michanganuo yake.

**Jedwali Na.7: Bajeti na Fedha za ruzuku ya miradi zilizotolewa hadi Juni, 2016**

HALMASHAURI	BAJETI IDHINISHWA		FEDHA TOLEWA			
	FEDHA ZA NDANI	FEDHA ZA NJE	FEDHA ZA NDANI	%	FEDHA ZA NJE	%
Mtwara Mikindani	385,348,000	1,701,352,000	31,875,000	8.27	963,399,000	56.63
Masasi Mji	1,330,634,000	294,504,000	0	0	337,358,000	114.55
Mtwara	1,847,219,000	474,323,000	48,895,000	2.65	586,949,000	123.74
Masasi	1,395,196,000	463,441,000	85,405,000	6.12	827,157,000	178.48
Nanyumbu	977,565,000	317,845,000	41,328,000	4.23	457,997,000	144.09
Newala	1,136,853,000	518,426,000	45,889,000	4.04	1,177,945,000	227.22
Tandahimba	1,217,536,000	565,942,000	46,991,000	3.86	508,248,000	89.81
<b>JUMLA</b>	<b>8,290,351,000</b>	<b>4,335,833,000</b>	<b>300,383,000</b>	<b>3.62</b>	<b>4,859,053,000</b>	<b>112.07</b>
<b>JUMLA KUU</b>	<b>12,626,184,000</b>		<b>5,159,436,000</b>			<b>40.86</b>

**Jedwali Na.8: Fedha za ruzuku ya miradi zilitolewa na zilizotumika hadi Juni, 2016**

HALMASHAURI	FEDHA TOLEWA		FEDHA TUMIKA			
	FEDHA ZA NDANI	FEDHA ZA NJE	FEDHA ZA NDANI	%	FEDHA ZA NJE	%
Mtwara Mikindani	31,875,000	963,399,000	25,375,000	79.61	527,251,000	54.73
Masasi Mji	0	337,358,000	0	0.00	282,302,000	83.68
Mtwara	48,895,000	586,949,000	33,006,000	67.50	210,942,000	35.94
Masasi	85,405,000	827,157,000	77,141,000	90.32	388,357,000	46.95
Nanyumbu	41,328,000	457,997,000	24,696,000	59.76	446,327,000	97.45
Newala	45,889,000	1,177,945,000	45,889,000	100.00	944,446,000	80.18
Tandahimba	46,991,000	508,248,000	46,991,000	100.00	416,702,000	81.99
<b>JUMLA</b>	<b>300,383,000</b>	<b>4,859,053,000</b>	<b>253,098,000</b>	<b>84.26</b>	<b>3,216,327,000</b>	<b>66.19</b>
<b>JUMLA KUU</b>	<b>5,159,436,000</b>		<b>3,469,425,000</b>			<b>67.24</b>

Pamoja na fedha hizo, Halmashauri zilipokea na kutumia fedha za TASAF na mfuko wa barabara kama inavyooneshwa katika jedwali namba 9.

**Jedwali Na.9: Fedha za Tasaf na Barabara zilizitolewa na kutumika 2015/16**

HALMASHAURI	MAPOKEZI		MATUMIZI			
	Barabara	Tasaf	Barabara	%	Tasaf	%
Mtwara Mikindani	903,305,000	602,142,000	493,222,000	54.60	602,142,000	100.00
Masasi Mji	936,536,000	705,303,000	843,516,000	90.07	705,158,000	99.98
Mtwara	1,585,116,000	2,373,997,000	1,223,240,000	77.17	2,360,881,000	99.45
Masasi	1,188,532,000	2,402,521,000	332,570,000	27.98	2,389,679,000	99.47
Nanyumbu	0	514,681,000	0	0	514,681,000	100.00
Newala	1,290,429,000	1,335,974,000	1,226,819,000	95.07	1,335,974,000	100.00
Tandahimba	695,894,000	1,553,294,000	602,147,000	86.53	1,464,992,000	94.32
<b>JUMLA</b>	<b>6,599,812,000</b>	<b>9,487,912,000</b>	<b>4,721,514,000</b>	<b>71.51</b>	<b>9,373,507,000</b>	<b>98.79</b>



### **2.3.3 Program/Miradi ya Maendeleo iliyotekelezwa hadi Juni, 2016.**

Orodha ya baadhi ya Program/Miradi ya Maendeleo iliyotekelezwa na Sekretarieti ya Mkoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa hadi Juni, 2016 ni pamoja na;

#### **a) Sekretarieti ya Mkoa**

- Kufuatilia utekelezaji wa programu za maji (RWSSP), usimamizi na ufuatiliaji wa sekta ya afya (HSBF), kufuatilia shughuli za mapambano dhidi ya Ukimwi katika mkoa.
- Utekelezaji wa programu ya menejimenti ya fedha za umma (PFMRP).

#### **b) Mamlaka za Serikali za Mitaa**

- Ujenzi wa miundombinu katika shule za Msingi na Sekondari.
- Ujenzi wa miundombinu mbalimbali ya afya.
- Kuendesha kampeni ya usafi wa mazingira.
- Ujenzi wa majengo mbalimbali ya ofisi kama ofisi za vijiji na kata.
- Utekelezaji wa programu za maji (RWSSP), elimu (SEDP), afya (HSBF), kilimo (ASDP) na mapambano dhidi ya Ukimwi.
- Ujenzi wa miundombinu ya barabara.
- Utekelezaji wa TASAF III

**3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA KIPINDI CHA JULAI HADI FEBRUARI, 2017-MWAKA 2016/2017**

**3.1 MADUHULI YA MKOA NA MAKUSANYO YA HALMASHAURI MWAKA 2016/17**

**3.1.1 Makadirio na Makusanyo ya Sekretarieti ya Mkoa kwa mwaka 2016/17**

Katika mwaka 2016/17 Sekretarieti ya Mkoa imeidhinishiwa kukusanya jumla ya shilingi **541,000.00** kutoka chanzo cha kodi ya pango katika nyumba tano za Serikali kama mapato ya Serikali yanayokwenda moja kwa moja Hazina. Hadi Februari, 2017 jumla ya shilingi **988,000.00** zimekusanywa sawa na **182.62%** ya makadirio.

**3.1.2 Makadirio na Makusanyo ya Halmashauri kwa mwaka 2016/17**

Katika mwaka 2016/17 Halmashauri zimeidhinishiwa kukusanya mapato ya ndani yenye jumla ya shilingi **25,171,728,000.00** kutoka vyanzo mbalimbali vya ndani. Hadi Februari, 2017 jumla ya shilingi **17,523,489,000.00** zimekusanywa sawa na **69.62%** ya lengo. Jedwali Na.10 linaonesha mchanganuo wake.

**Jedwali Na.10: Makadirio na Makusanyo ya Halmashauri hadi Februari, 2017**

HALMASHAURI	MAKADIRIO	MAKUSANYO HADI FEBRUARI, 2017			
		MAKUSANYO YASIYOLINDWA	MAKUSANYO LINDWA	JUMLA	%
Mtwara Mikindani	4,542,968,000	2,589,870,000	140,655,000	2,730,525,000	<b>60.10</b>
Masasi Mji	1,867,104,000	1,044,209,000	221,109,000	1,265,318,000	<b>67.77</b>
Newala Mji	1,939,486,000	831,238,000	254,821,000	1,086,059,000	<b>55.99</b>
Nanyamba Mji	1,226,868,000	1,167,464,000	27,082,000	1,194,546,000	<b>97.36</b>
Mtwara	2,306,244,000	1,106,606,000	12,000,000	1,118,606,000	<b>48.50</b>
Masasi	4,003,191,000	1,875,926,000	84,146,000	1,960,072,000	<b>48.96</b>
Nanyumbu	2,407,389,000	1,444,778,000	568,389,000	2,013,167,000	<b>83.62</b>
Newala	1,996,264,000	1,162,739,000	336,948,000	1,499,687,000	<b>75.12</b>
Tandahimba	4,882,214,000	3,774,852,000	880,657,000	4,655,509,000	<b>95.35</b>
<b>JUMLA</b>	<b>25,171,728,000</b>	<b>14,997,682,000</b>	<b>2,525,807,000</b>	<b>17,523,489,000</b>	<b>69.62</b>

**Nyongeza:** Makusanyo lindwa ni mapato yanayojumuisha vyanzo vya ada ya huduma (user fee), mfuko wa afya ya jamii (CHF), mfuko wa elimu na export levy. Matumizi ya fedha hizi huzingatia sheria CHF, Mfuko wa elimu na miongozo ya cost sharing na export levy.

Halmashauri hazikuweza kufikia wastani wa malengo ya makusanyo kwa kipindi cha nusu mwaka kutokana na;

- Kuchelewa kuidhinishwa kwa sheria ndogo.
- Kodi ya majengo kukusanywa na TRA.
- Wizara ya ardhi kutotoa marejesho ya 30%.

Matumizi mapato ya ndani katika miradi ya maendeleo kwa makusanyo yasiyolindwa ni kama inavyooneshwa katika jedwali namba 11 ambapo jumla ya sh. **1,100,990,000 (73.41%)** za wanawake na vijana zimetengwa kati ya sh. **1,499,769,000** zilizotakiwa na miradi mingine ya maendeleo jumla y ash. **4,952,237,000 (68.06%)** zimetengwa kati ya sh. **7,275,882,000** zilizotakiwa.

**Jedwali Na.11: Matumizi ya makusanyo yasiyolindwa hadi Februari, 2017**

HALMASHAURI	MAKUSANYO YASIYOLINDWA	Wanawake na Vijana (10%)				Miradi ya Maendeleo (50%)			
		Takiwa	%	Tolewa	%	Takiwa	%	Tolewa	%
Mtwara MC	2,589,870,000	258,987,000	10	258,987,000	100.00	1,071,976,000	50	943,404,000	88.00
Masasi TC	1,044,209,000	104,421,000	10	68,966,000	66.05	522,105,000	50	206,338,000	39.52
Newala TC	831,238,000	83,124,000	10	64,729,000	77.87	415,619,000	50	371,802,000	89.45
Nanyamba TC	1,167,464,000	116,746,000	10	104,725,000	89.70	583,732,000	50	431,660,000	73.95
Mtwara	1,106,606,000	110,661,000	10	52,740,000	47.66	553,303,000	50	418,329,000	75.61
Masasi	1,875,926,000	187,593,000	10	187,024,000	99.69	937,963,000	50	351,902,000	37.51
Nanyumbu	1,444,778,000	144,478,000	10	107,000,000	74.06	722,389,000	50	722,389,000	100.0
Newala	1,162,739,000	116,274,000	10	50,000,000	43.00	581,369,000	50	255,225,000	43.90
Tandahimba	3,774,852,000	377,485,000	10	206,819,000	54.78	1,887,426,000	50	1,251,188,000	66.29
<b>JUMLA</b>	<b>14,997,682,000</b>	<b>1,499,769,000</b>	<b>10</b>	<b>1,100,990,000</b>	<b>73.41</b>	<b>7,275,882,000</b>	<b>50</b>	<b>4,952,237,000</b>	<b>68.06</b>

**Nyongeza:** Idadi ya vikundi vilivyokopeshwa imeaoneshwa katika kiambatisho namba 1 na orodha ya vikundi imeoneshwa katika kiambatisho namba 2.

### 3.2 FEDHA ZA RUZUKU KWA MATUMIZI YA KAWAIDA MWAKA 2016/2017

#### 3.2.1 Fedha zilizoidhinishwa na kutolewa kwa Sekretarieti ya Mkoa mwaka 2016/17

Katika mwaka 2016/17 Sekretarieti ya Mkoa iliidhinishwa jumla ya shilingi **6,930,724,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida ili kugharamia maeneo ya mishahara na matumizi mengineyo. Fedha zilizotolewa hadi Februari, 2017 ni jumla ya shilingi **4,291,935,000.00** sawa na **61.93%** ya bajeti iliyoidhinishwa. Aidha, kiasi kilichotumika ni shilingi **4,291,935,000.00** sawa na **100.00%** ya fedha zilizotolewa. Jedwali Na.12 linaonesha mchanganuo wake.

**Jedwali Na.12: Bajeti, Fedha zilizotolewa na kutumika hadi Februari, 2017**

KASMA	BAJETI	FEDHA TOLEWA		FEDHA TUMIKA	
		KIASI	%	KIASI	%
Mishahara	5,372,873,000	3,218,787,000	56.91	3,218,787,000	100.00
Matumizi Mengineyo	1,557,851,000	1,073,148,000	68.89	1,073,148,000	100.00
<b>JUMLA</b>	<b>6,930,724,000</b>	<b>4,291,935,000</b>	<b>61.93</b>	<b>4,291,935,000</b>	<b>100.00</b>

**Nyongeza:** Sekretarieti ya Mkoa ilipokea jumla ya sh. **393,349,000** kwa ajili ya kulipa madeni mbalimbali ikiwa madeni ya wazabuni sh. **31,802,000** na madeni ya watumishi sh. **361,547,000**.

#### 3.2.2 Fedha zilizoidhinishwa na kutolewa kwa Halmashauri mwaka 2016/17

Katika mwaka 2016/17 Halmashauri zimeidhinishwa kukusanya fedha za ruzuku zenye jumla ya shilingi **119,321,760,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida ili kugharamia maeneo ya mishahara na matumizi mengineyo. Fedha zilizotolewa hadi Februari, 2017 ni jumla ya shilingi **78,749,462,000.00** sawa na **65.99%** ya makadirio. Aidha, kiasi kilichotumika ni shilingi **78,749,462,000.00** sawa na **100.00%** ya fedha zilizopokelewa Jedwali Na.13 na 14 yanaonesha michanganuo yake.

**Jedwali Na.13: Bajeti na Mapokezi ya fedha za Matumizi ya Kawaida hadi Februari, 2017**

HALMASHAURI	BAJETI		FEDHA TOLEWA			
	MISHAHARA	MATUMIZI MENGINEYO	MISHAHARA	%	MATUMIZI MENGINEYO	%
Mtwara Mikindani	13,153,215,000	1,713,189,000	8,488,586,000	64.54	1,021,191,000	59.61
Masasi Mji	11,384,584,000	1,104,861,000	7,348,458,000	64.55	582,299,000	52.70
Newala Mji	0	723,213,000	76,696,000	N/A	291,664,000	40.33
Nanyamba Mji	0	668,755,000	3,701,132,000	N/A	417,051,000	62.36
Mtwara	18,827,274,000	1,168,524,000	8,554,254,000	45.44	740,309,000	63.35
Masasi	17,886,733,000	2,483,310,000	11,857,022,000	66.29	1,439,454,000	57.97
Nanyumbu	9,351,546,000	751,114,000	8,120,769,000	86.84	509,804,000	67.87
Newala	18,391,530,000	721,251,000	11,604,776,000	63.10	500,943,000	69.45
Tandahimba	19,536,773,000	1,455,888,000	12,635,072,000	64.67	859,982,000	59.07
<b>JUMLA</b>	<b>108,531,655,000</b>	<b>10,790,105,000</b>	<b>72,386,765,000</b>	<b>66.70</b>	<b>6,362,697,000</b>	<b>58.97</b>
	<b>119,321,760,000</b>		<b>78,749,462,000</b>			<b>65.99</b>

**Nyongeza:** Asilimia ya fedha za mishahara zilizotolewa kwa Newala Mji na Nanyamba Mji hazipo kutokana na halmshauri hizo mpya kutokuwa na makadirio ya bajeti ya mishahara.

**Jedwali Na.14: Fedha zilizotolewa na kutumika kwa Matumizi ya kawaida hadi Feb, 2017**

HALMASHAURI	FEDHA ZILIZOTOLEWA		FEDHA ZILIZOTUMIKA			
	MISHAHARA	MATUMIZI MENGINEYO	MISHAHARA	%	MATUMIZI MENGINEYO	%
Mtwara Mikindani	8,488,586,000	1,021,191,000	8,488,586,000	100.00	1,021,191,000	100.00
Masasi Mji	7,348,458,000	582,299,000	7,348,458,000	100.00	582,299,000	100.00
Newala Mji	76,696,000	291,664,000	76,696,000	100.00	291,664,000	100.00
Nanyamba Mji	3,701,132,000	417,051,000	3,701,132,000	100.00	417,051,000	100.00
Mtwara	8,554,254,000	740,309,000	8,554,254,000	100.00	740,309,000	100.00
Masasi	11,857,022,000	1,439,454,000	11,857,022,000	100.00	1,439,454,000	100.00
Nanyumbu	8,120,769,000	509,804,000	8,120,769,000	100.00	509,804,000	100.00
Newala	11,604,776,000	500,943,000	11,604,776,000	100.00	500,943,000	100.00
Tandahimba	12,635,072,000	859,982,000	12,635,072,000	100.00	859,982,000	100.00
<b>JUMLA</b>	<b>72,386,765,000</b>	<b>6,362,697,000</b>	<b>72,386,765,000</b>	<b>100.00</b>	<b>6,362,697,000</b>	<b>100.00</b>
	<b>78,749,462,000</b>		<b>78,749,462,000</b>			<b>100.00</b>

**3.2.3 Shughuli zilizotekelezwa hadi Februari, 2017**

Orodha ya baadhi ya shughuli zilizotekelezwa na Sekretarieti ya Mkoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa hadi Februari, 2017 ni pamoja na;

**a) Sekretarieti ya Mkoa**

- Kusimamia masuala ya ulinzi na usalama ndani ya Mkoa.
- Kuendesha vikao vya mbalimbali vya kisheria.
- Kutoa ushauri wa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa.
- Kuratibu shughuli mbalimbali za Serikali za kila siku za kutoa huduma kwa wananchi.
- Kulipa mishahara kwa watumishi.
- Kuratibu uendeshaji wa mitihani ya elimu msingi na sekondari.
- Kuratibu ziara za viongozi mbalimbali wa Mkoa na kitaifa.
- Kufanya ufuatiliaji wa shughuli zilizotekelezwa na Halmashauri.
- Kutoa huduma za tiba na kinga katika hospitali ya Mkoa.

**b) Mamlaka za Serikali za Mitaa**

- Kulipa mishahara kwa watumishi wote.
- Kufanya ufuatiliaji na usimamizi wa shughuli zilizotekelezwa katika Kata, Vijiji/Mitaa na Vitongoji.
- Kutoa huduma mbalimbali za kila siku kwa wananchi.
- Kuendesha vikao vya mbalimbali vya kisheria.
- Uendeshaji wa mitihani ya elimu msingi na sekondari.
- Uandikishaji wanafunzi na utoaji wa elimu ya msingi na sekondari ulifanyika.

### **3.4 FEDHA ZA RUZUKU KWA MIRADI YA MAENDELEO MWAKA 2016/2017**

#### **3.4.1 Fedha zilizoidhinishwa na kutolewa kwa Sekretarieti ya Mkoa mwaka 2016/17**

Katika mwaka 2016/17 Sekretarieti ya Mkoa imeidhinishiwa jumla ya shilingi **1,577,566,000.00** ili kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi **1,110,000,000.00 (70.40%)** ni fedha za ndani na shilingi **467,566,000.00 (29.60%)** ni fedha za nje. Hadi kufikia Februari, 2017 jumla ya shilingi **905,117,000.00** zimetolewa sawa na **57.37%** ya bajeti idhinishwa. Aidha, kiasi kilichotumika ni shilingi **263,601,000.00** sawa na **29.12%** ya fedha zilizopokelewa. Jedwali Na.15 linaonesha mchanganuo wake.

**Jedwali Na.15. Bajeti, Fedha zilizotolewa na kutumika hadi Feb, 2017**

KASMA	BAJETI	FEDHA TOLEWA		FEDHA TUMIKA	
		KIASI	%	KIASI	%
Fedha za Ndani	1,110,000,000	555,000,000	50.00	66,710,000	12.01
Fedha za Nje	467,566,000	350,117,000	74.88	196,891,000	56.23
<b>JUMLA</b>	<b>1,577,566,000</b>	<b>905,117,000</b>	<b>57.37</b>	<b>263,601,000</b>	<b>29.12</b>

#### **3.4.2 Fedha zilizoidhinishwa na kutolewa kwa Halmashauri 2016/17**

Katika mwaka 2016/17 Halmashauri zimeidhinishiwa fedha za ruzuku jumla ya shilingi **19,866,655,000.00** ili kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi **11,288,344,000.00 (56.82%)** ni fedha za ndani na shilingi **8,578,311,000.00 (43.18%)** ni fedha za nje. Hadi kufikia Februari, 2017 jumla ya shilingi **7,126,087,000.00** zimetolewa sawa na **35.86%** ya makadirio. Aidha, kiasi kilichotumika ni shilingi **3,023,651,000.00** sawa na **42.43%** ya fedha zilizopokelewa. Jedwali Na.16 na 17 yanaonesha michanganuo yake.

**Jedwali Na.16. Bajeti na Fedha za ruzuku ya miradi zilizotolewa hadi Feb, 2017**

HALMASHAURI	BAJETI IDHINISHWA		FEDHA TOLEWA			
	FEDHA ZA NDANI	FEDHA ZA NJE	FEDHA ZA NDANI	%	FEDHA ZA NJE	%
Mtwara Mikindani	570,526,000	3,349,663,000	183,645,000	<b>32.19</b>	166,482,000	<b>4.97</b>
Masasi Mji	1,284,760,000	719,561,000	926,599,000	<b>72.12</b>	198,669,000	<b>27.61</b>
Newala Mji	2,487,749,000	111,619,000	645,844,000	<b>25.96</b>	93,714,000	<b>83.96</b>
Nanyamba Mji	2,556,219,000	366,832,000	673,299,000	<b>26.34</b>	191,374,000	<b>52.17</b>
Mtwara	1,271,703,000	526,370,000	958,763,000	<b>75.39</b>	243,466,000	<b>46.25</b>
Masasi	1,111,686,000	888,617,000	375,945,000	<b>33.82</b>	463,865,000	<b>52.20</b>
Nanyumbu	584,281,000	657,913,000	230,281,000	<b>39.41</b>	605,969,000	<b>92.10</b>
Newala	455,578,000	595,576,000	184,569,000	<b>40.51</b>	265,858,000	<b>44.64</b>
Tandahimba	965,842,000	1,362,160,000	329,590,000	<b>34.12</b>	388,154,000	<b>28.50</b>
<b>JUMLA</b>	<b>11,288,344,000</b>	<b>8,578,311,000</b>	<b>4,508,535,000</b>	<b>39.94</b>	<b>2,617,552,000</b>	<b>30.51</b>
<b>JUMLA KUU</b>	<b>19,866,655,000</b>		<b>7,126,087,000</b>			<b>35.86</b>

**Jedwali Na.17: Fedha za ruzuku ya miradi zilitolewa na zilizotumika hadi Feb, 2017**

HALMASHAURI	FEDHA TOLEWA		FEDHA TUMIKA			
	FEDHA ZA NDANI	FEDHA ZA NJE	FEDHA ZA NDANI	%	FEDHA ZA NJE	%
Mtwara Mikindani	183,645,000	166,482,000	119,859,000	<b>65.27</b>	109,748,000	<b>65.92</b>
Masasi Mji	926,599,000	198,669,000	124,433,000	<b>13.43</b>	108,980,000	<b>54.86</b>
Newala Mji	645,844,000	93,714,000	145,844,000	<b>22.58</b>	18,234,000	<b>19.45</b>
Nanyamba Mji	673,299,000	191,374,000	257,155,000	<b>38.19</b>	104,846,000	<b>54.78</b>
Mtwara	958,763,000	243,466,000	162,129,000	<b>16.91</b>	243,466,000	<b>100.00</b>
Masasi	375,945,000	463,865,000	308,647,000	<b>82.09</b>	141,773,000	<b>30.56</b>
Nanyumbu	230,281,000	605,969,000	144,182,000	<b>62.61</b>	324,816,000	<b>53.60</b>
Newala	184,569,000	265,858,000	88,899,000	<b>48.16</b>	134,875,000	<b>50.73</b>
Tandahimba	329,590,000	388,154,000	261,666,000	<b>79.39</b>	224,099,000	<b>57.73</b>
<b>JUMLA</b>	<b>4,508,535,000</b>	<b>2,617,552,000</b>	<b>1,612,814,000</b>	<b>35.77</b>	<b>1,410,837,000</b>	<b>87.48</b>
<b>JUMLA KUU</b>	<b>7,126,087,000</b>		<b>3,023,651,000</b>			<b>42.43</b>

Pamoja na fedha hizo Halmashauri zimepokea fedha nje ya bajeti kama inavyooneshwa katika jedwali namba 18.



**Jedwali Na.18: Fedha za Tasaf na Barabara zilizitolewa na kutumika hadi Feb, 2017**

HALMASHAURI	MAPOKEZI		MATUMIZI			
	Barabara	Tasaf	Barabara	%	Tasaf	%
Mtwara Mikindani	1,168,287,000	277,523,000	782,074,000	<b>66.94</b>	255,325,000	<b>92.00</b>
Masasi Mji	258,123,000	406,380,000	215,849,000	<b>83.62</b>	354,478,000	<b>87.23</b>
Mtwara	886,014,000	1,787,665,000	886,014,000	<b>100.00</b>	1,473,334,000	<b>82.42</b>
Masasi	144,981,000	1,866,766,000	2,213,000	<b>1.52</b>	1,451,579,000	<b>77.75</b>
Nanyumbu	453,819,000	1,309,454,000	321,644,000	<b>70.87</b>	1,090,869,000	<b>83.31</b>
Newala	472,455,000	1,099,831,000	446,063,000	<b>94.41</b>	540,470,000	<b>49.14</b>
Tandahimba	611,148,000	1,019,832,000	337,110,000	<b>55.16</b>	934,755,000	<b>91.66</b>
<b>JUMLA</b>	<b>3,994,827,000</b>	<b>7,767,451,000</b>	<b>2,990,967,000</b>	<b>74.87</b>	<b>6,100,810,000</b>	<b>78.54</b>

**3.4.3 Program/Miradi ya Maendeleo iliyotekelezwa hadi Februari, 2017.**

Orodha ya baadhi ya program/miradi ya maendeleo iliyotekelezwa na Sekretarieti ya Mkoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa hadi Februari, 2017 ni pamoja na;

**a) Sekretarieti ya Mkoa**

- Kufuatilia utekelezaji wa programu za maji (RWSSP), usimamizi na ufuatiliaji wa sekta ya afya (HSBF).
- Utekelezaji wa programu ya menejimenti ya fedha za umma (PFMRP).

**b) Mamlaka za Serikali za Mitaa**

- Ujenzi wa miundombinu katika shule za Msingi na Sekondari.
- Ujenzi wa miundombinu mbalimbali ya afya.
- Kuendesha kampeni ya usafi wa mazingira.
- Utekelezaji wa programu za maji (RWSSP), elimu (SEDP), afya (HSBF)
- Ujenzi wa miundombinu ya barabara.

### **3.5 CHANGAMOTO ZILIZOJITokeza WAKATI WA UTEKELEZAJI WA BAJETI**

Changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa bajeti kwa nusu mwaka 2016/17 kwa Sekretarieti ya Mkoa na Halmashauri ni pamoja na:

- Fedha za miradi kutotolewa kwa wakati.
- Kutokutolewa kwa fedha za matumizi mengineyo katika baadhi ya miezi kwa Halmashauri.
- Kutolewa fedha kidogo kwa ajili matumizi mengineyo.

### **3.6 MAPENDEKEZO**

Kutokana na changamoto zilizojitokeza, Mkoa unapendekeza yafuatayo;-

- Mkoa uongezewe bajeti yake kulingana na mahitaji halisi yanayoendana na nafasi ya Mkoa katika kuongoza maendeleo na mabadiliko makubwa yatakayobadili taswira ya uchumi wa nchi.
- Mazingira ya utendaji kazi kwa mkoa wa Mtwara unaotarajiwa kupokea, kuhudumia na kuwezesha uwekezaji mkubwa kwa manufaa ya Taifa, kunahitajika vitendea kazi na mazingira bora ya majengo ili kuleta ufanisi. Mazingira bora ya kazi ni motisha kubwa kwa watumishi kupenda kuja kufanya kazi Mtwara.
- Fedha zote zinazoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Mkoa zitolewe kwa wakati ili mipango ya maendeleo na shughuli za uendeshaji katika Mkoa na Halmashauri zake zitekelezwe bila vikwazo sambamba na kazi ya uwekezaji.

### **4.0 MAAGIZO YA KAMATI YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA**

Katika kikao cha kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fungu 80 Mkoa wa Mtwara kwa mwaka 2016/2017 kilichofanyika tarehe 12/04/2016 katika ukumbi wa Mwalimu Nyerere Dar es salaam, Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa ilitoa hoja mbalimbali ambapo hoja hizo zilijibiwa wakati wa kikao. Kamati

haikutoa maagizo mahsusi kwa Mkoa ili kuyatekeleza na kuyatolea taarifa katika kikao kinachofuata.

## 5.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

### 5.1 MADUHULI YA MKOA NA MAKUSANYO YA HALMASHAURI.

